**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI BWIRU WAVULANA**

S.L.P 217,
ILEMELA,
**MWANZA**

Kumb. Na. BBTSS/ADM/2026 TAREHE_________

Email: bwiruboyssecondaryschool1920@gmail.com
Website: http://bwiruboystech.sc.tz
**MKUU WA SHULE 0626 245451**
**MAKAMU MKUU WA SHULE 0769 575630**
**MTAALUMA 0620 825823**
**MALEZI 0685 906820**
**PATRON 0620 534545**

JINA LA MWANAFUNZI__________________________________________ (JINAKAMILI)
S.L.P ___________________________
_______________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2026 SHULE YA UFUNDI BWIRU WAVULANA**
**WILAYA YA ILEMELA MKOA WA MWANZA**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka **2026** katika shule ya sekondari ya **Ufundi Bwiru Wavulana**. Hongera na karibu sana. Shule itafunguliwa tarehe **13/01/2026** na masomo yataanza tarehe **14/01/2026.**

**MUDA WA KURIPOTI SHULENI**

Mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni siku za kazi tu, jumatatu hadi ijumaa muda wa kupokelewa ni saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

**NAMNA YA KUFIKA SHULENI**

(1) Shule ipo kilometa 8 kutoka katikati ya jiji la mwanza, katika wilaya ya ilemela .ukifika stendi ya mabasi ya nyegezi au Buzuruga, panda daladala zinazoenda mjini Mwanza, kisha uliza stendi ya daladala **ziendazo Bwiru**. Kama utakuja kwa treni au meli pia uliza

stendi ya daladala ziendazo **Bwiru**. Stendi hii iko mtaa wa **Makoroboi**. Ukichukua usafiri wa daladala, shuka kituo cha mwisho kabisa (**Bwiru wavulana** ) zinapogeukia daladala hizo.

**(2)** Fika shuleni kwa tarehe iliyopangwa na fomu hii. Hakuna sababu itakayokubalika kwa mtoto yeyote kutofika shuleni mapema. Hali kadhalika jiepushe na aibu ya kuumbuka kwa kuja shuleni kwa jina la mtu mwingine**.**

**MAHITAJI YAKUJANAYO**

**(1) (A) VIFAA VYA TAALUMA**

(i) Madaftari kumi (10) kaunta books quire three.
(ii) Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical instrument set) aina ya **NATARAJ.**
(iii) Mathematical table (Four figure ).

**(2) SARE ZA SHULE**

(i) Mashati mawili meupe mikono mifupi
(ii) Suruali nyeusi mbili zenye malinda mawili , mifuko mitatu zisiwe za kubana au buga.**(Zinapatikana shuleni).**
(iii) Ovalori la rangi ya dark blue.**(Zinapatikana shuleni).**
(iv) Tisheti mbili za rangi ya damu ya mzee zenye kola.(**Zinapatikana shuleni tu zikiwa na nembo ya shule).**
(v) Jozi ya viatu vya ngozi vya kamba vyenye visigino vifupi, kiwi nyeusi na brush ya viatu
(vi) Jozi mbili za soksi ndefu nyeupe bila urembo wowote
(vii) Sweta ya rangi ya blue yenye nembo ya shule **(zinapatikana shuleni tu zikiwa na nembo ya shule).**
(viii) Tracksuit za rangi ya dark blue zenye nembo ya shule. **(zinapatikana shuleni tu zikiwa na nembo ya shule).**
(ix) Michezo ni afya, Nguo za michezo, mazoezi na mchakamchaka zinapatikana shuleni **zikiwa na nembo ya shule.**

**(3) VIFAA VYA USAFI BINAFSI**

(i) Ndoo ndogo moja ya kuogea, chombo cha kuhifadhia maji safi ya kunywa ( dumu la lita 5)
(ii) Vifaa vya usafi binafsi kama mswaki, dawa ya meno, mafuta , toilet paper 5, sabuni za kuogea na sabuni za kufuria
(iii) Kandambili za kuogea aina ya yeboyebo.

**(4) VIFAA BINAFSI VINGINEVYO**

(i) Chandarua na awe na utamaduni wa kukitibu kwa dawa.
(ii) Vifaa vya kulia chakula, bakuli, sahani , kikombe cha uji nusu lita, kijiko n.k.
(iii) Tochi ndogo moja imara na betri zake.
(iv) Godoro futi 2½ kwa sita.
(v) Shuka mbili za rangi ya light blue za kutandika na kujifunika, mto mmoja na blanketi moja zito pamoja na sanduku la chuma au bati lisiwe begi.
(vi) Bukta nyeusi na raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

**NB: VIFAA VIFUATAVYO VINAPATIKANA KATIKA MADUKA YALIYOPO MAENEO YA SHULE WAKATI NA TAREHE WANAFUNZI WANAPORIPOTI.**
**( mzazi anaweza kuja na pesa ili kupunguza mizigo na usumbufu).**

| NA | KIFAA | IDADI | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| 1 | Tisheti zenye nembo ya shule. | PC 1 | 14,000/= |
| 2 | Sweta la shule lenye nembo ya shule. | PC 1 | 15,000/= |
| 3 | Suruali ya shule zinapatikana shuleni. | PC 1 | 18,000/= |
| 4 | Shuka (light blue) zinapatikana shuleni. | PC 1 | 8,000/= |
| 5 | Ovalori (dark blue) zinapatikana shuleni. | PC 1 | 25,000/= |
| 6 | Tracksuit zinapatikana shuleni. | PC 1 | 23,000/= |
| 7 | Godoro futi $2\frac{1}{2}$ (deluxe ) | PC 1 | 45,000/= |
| 8 | Chandarua (Net) | PC 1 | 7,500/= |
| 9 | Ndoo ndogo ya kuogea/kufulia | PC 1 | 4,500/= |
| 10 | Dumu la lita 5 la kuhifadhia maji ya kunywa | PC 1 | 3,000/= |

**(5) VITU VISIVYO RUHUSIWA SHULENI**

Soma nyongeza **A** ya sheria za shule ambayo imeambatanishwa.

**MAAGIZO MENGINE:**

1. **FEDHA YA MATUMIZI:**
   Wanafunzi hawaruhusiwi kwenda mjini. Mzazi ahakikishe anamnunulia kijana wake mahitaji muhimu, pia ampe pesa kiasi cha shilingi 20,000/= kwa ajili ya mahitaji madogomadogo ambayo hupatikana katika maduka yaliyopo katika eneo la shuleni.

2. **FEDHA ZA MATIBABU**
   Gharama zote za matibabu zitagharamiwa na mzazi. Hivyo mzazi/mlezi amwandalie mwanafunzi **<u>kadi ya bima ya afya na aje nayo siku ya kuripoti.</u>**

**<u>NB:</u> MZAZI AU MLEZI UNAWEZA KUJA NA SH 50,400/= UKAMLIPIA MWANAFUNZI ILI AANDALIWE KADI YA BIMA YA AFYA KAMA HANA.**

3. **NAULI**
   Mzazi ampe mtoto wake nauli ya kumrudisha nyumbani kila mwisho wa mhula. Shule haitoi huduma ya chakula, malazi wakati shule zinapofungwa katika likizo kubwa.
4. **VYETI BANDIA VYA HOSPITALI:**
   Baadhi ya wazazi hushirikiana na watoto wao kutafuta taarifa bandia ili wasifanye kazi za shule au kula vyakula aina Fulani. mzazi au mtoto asifanye hivyo kwa kuwa mazingira hayatamfaa kujifunza.

5. **KUJAZA FOMU:**
   Siku ya kuwasili shuleni kwa mara ya kwanza, mwanafunzi atatakiwa kuleta barua hii pamoja na fomu zilizotajwa hapo chini zikiwa zimejazwa kikamilifu.

   a) **Nyongeza B: AFYA YA MWANAFUNZI.**
   Fomu hii ijazwe kikamilifu na kugongwa mhuri wa Daktari wa Hospitali ya serikali ya wilaya, Mkoa au Rufaa. Taarifa ya mganga atakayejaza fomu hii itakuwa kielelezo pekee kitakachokubalika shuleni kuhusiana na afya ya mtoto. Hatupokei taarifa ya afya toka hospitali isiyo ya Serikali.

   b) **Nyongeza Na. C: HISTORIA KAMILI YA MWANAFUNZI.**
   Historia kamili ya mwanafunzi na maelezo yake binafsi yajazwe na Mzazi/ Mlezi kwa ufasaha kwa ajili ya kumbukumbu za shule.

   c) **Nyongeza Na. D: NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI.**
   Mzazi/Mlezi aorodheshe ndugu wa karibu watatu watakaomwona na pia atakaokwenda yeye au shule kufanya nao mawasiliano kwa niaba ya Mzazi/Mlezi.

   d) **Nyongeza Na. E: UTII WA SHERIA.**
   Hali kadhalika, ahadi ya kutii sheria, amri na mamlaka ya shule ijazwe kikamilifu.

   e) Mzazi/mlezi alete nakala ya **<u>cheti cha kuzaliwa</u>** (photocopy of birth certificate) cha mtoto au cheti cha uraia endapo mwanafunzi si raia wa nchi hii.

f) Pia mzazi alete **picha yake moja,** Ndugu wa karibu au mlezi pamoja na namba zao za simu. Ili kurahisisha mawasiliano pindi kunauhitaji wao mfano ugonjwa, utovu wa nidhamu n.k.

g) Pia mzazi/mlezi amwandalie mwanafunzi **kadi ya bima ya Afya** na aje nayo siku ya kuripoti.

**MIPAKA YA SHULE**

**MASHARIKI**

Nyumba za watumishi wa shule, daraja kati ya shule yetu na shule ya **sekondari kitangili.**

**KUSINI**

Barabara itokayo mjini kuelekea shule ya sekondari ya **wasichana bwiru.**

**MAGHARIBI**

Barabara kati ya shule yetu na shule ya **msingi bwiru.**

**KASKAZINI**

Mwisho wa majengo ya shule yaliyoko nyuma ya jiko la shule. Mpaka ni **shule ya sekondari Mnarani na Bwiru Wavulana.**

Ni kosa kwa mwanafunzi kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Ruhusa ya kutoka nje ya eneo la shule ni lazima ipatikane kutoka kwa mwalimu wa zamu ambaye atatoa karatasi maalum ya ruhusa. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na makamu mkuu wa shule baada ya kupelekwa maombi kupitia kwa mlezi wa nyumba na mwalimu wa zamu anayehusika. Mwanafunzi aliyeruhusiwa kwenda nje ya mipaka ya shule lazima avae sare ya shule.

**Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:**

(i) Jikoni.
(ii) Nyumba za watumishi wote wa shule.

**Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo.Akikamatwa anafukuzwa shule.**

(i) Vilabu vya pombe
(ii) Nyumba za starehe kama dansi, filamu au video n.k.
(iii) Nyumba za kulala wageni

**1. SARE ZA SHULE**

(i) Wakati wa masomo (vipindi darasani) wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare kamili ya shule (suruali nyeusi , shati jeupe na sweta la shule ).

(ii) Baada ya vipindi na siku zisizokuwa za masomo, wanafunzi wanatakiwa kuvaa nguo zilizoruhusiwa tu. (Tisheti,tracksuit zenye nembo ya shule na suruali nyeusi tu mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani shuleni).

**2. UTARATIBU WA MABWENI**

(i) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa bwenini wakati wa vipindi madarasani, vipindi vya kujisomea (usiku). Na shughuli nyingine za kishule nje ya madarasa isipokuwa kwa ruhusa maalum.
(ii) Bweni lazima lisafishwe kila siku asubuhi na wanafunzi wote lazima watandike vizuri vitanda vyao kabla ya kwenda darasani.
(iii) Mgeni yeyote haruhusiwi kuingia kwenye mabweni ya wanafunzi.
(iv) Radio zote na vyombo vingine vya muziki, mabwenini vifungwe baada ya kuzima taa na wanafunzi wote lazima wawe kimya wamelala.
(v) Ni marufuku kubandika picha kwenye kuta za mabweni, madarasa na sehemu nyingine zizungukazo mazingira ya shule hii na sehemu nyingine nje ya shule.

Mimi mzazi/mlezi (jina kamili) …………………………………………. nimeelewa na kuzingatia taratibu zote hapo juu.

**Sahihi………………………** **tarehe………………………………**

**3. SHERIA ZA MADARASANI**

(i) Lazima kuwahi darasani na kukaa kimya muda wote
(ii) Hairuhusiwi kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi yeyote aliyemo darasani.
(iii) Akitaka kuuliza swali au kujibu swali mwanafunzi anyooshe mkono na kusimama baada ya kuruhusiwa kufanya hivyo.
(iv) Kila mwanafunzi ahudhulie vipindi vyote.
(v) Kila mwanafunzi atunze usafi wa darasa lake.

**4. MBAO ZA MATANGAZO**

(i) Ni marufuku mwanafunzi kuondoa au kuweka tangazo lolote katika mbao zozote za matangazo shuleni bila ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu.

**5. UPOKEAJI WA WAGENI**

(i) Wazazi/walezi wanaruhusiwa kutembelea shule kwa shida maalumu tu.
(ii) Wageni wote wa wanafunzi waripoti kwenye ofisi ya makarani/mwalimu wa zamu na mwanafunzi anayehusika ataitwa aonane nae.
(iii) Mzazi haruhusiwi kumletea chakula cha aina yeyote mwanafunzi.

**6. BARUA ZA WANAFUNZI**

(i) Barua zote za kiofisi za wanafunzi lazima zipitie kwa mkuu wa shule.

(ii) Mhudumu wa ofisi atakuwa na madaraka ya kuchukua barua, vifurushi na hati zote za fedha kutoka kwa wahusika ambao itabidi waonyeshe vitambulisho na kutia sahihi kuthibitisha kuwa wamepokea.

**7. SIMU.**

- Wanafunzi wote **hawaruhusiwi kuja na simu shuleni** akikamatwa nayo atafukuzwa shule .
- Mawasiliano yote kati ya mzazi/mlezi na shule yatafanywa na Mkuu wa Shule, Makamu wa mkuu wa shule,mlezi Elimu maalum(mahitaji maalum) na Ofisi ya taaluma tu.**Hairuhusiwi kupiga simu kwa mtumishi asiyehusika.**

**8. MAGONJWA**

(i) Mwanafunzi akiugua atoe taarifa haraka kwa mwalimu wa afya ili asaidiwe.Wanafunzi wenye maradhi ya muda mrefu kama pumu ama allergy watoe taarifa mara wafikapo shuleni.

**OFISI YA RAISI (TAMISEMI)**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI BWIRU WAVULANA**
**SHERIA ZA SHULE NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**
**NYONGEZA 'A'**

## 1.0.UTANGULIZI:

Sheria na kanuni muhimu za shule ni mwongozo wa utaratibu wa kuishi kwa jamii iliyopo hapa shuleni ili kufanikisha maendeleo ya shule. Mafanikio ya maendeleo ya shule yanategemeana sana jinsi mwanafunzi anavyotii na kuheshimu sheria na kanuni zilizowekwa. Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu Sayansi, Tecknolojia na ufundi, yenye zamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS ((Tamisemi) yenye majukumu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu.

### 1.1.MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA MUDA WOTE.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
**(c)** Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni ( preparation):
**(d)** Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
**(e)** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
**(f)** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
**(g)** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
**(h)** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ; na
**(i)** Kutunza mali za umma.

### 1.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE MARA MOJA.

Makosa yafuatayo yakitendwa yatamfanya mwanafunzi afutwe shule mara moja bila kujali ametenda kosa kwa mara ya kwanza / pili/tatu.

1. Wizi.
2. Uasherati au Ushoga,
3. Ubakaji,
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
5. Kupigana, kupiga au kusababisha wanafunzi kupigana.
6. Kutishia kumpiga mlezi/Mwalimu.

7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendela ya Taifa.
9. Kuoa.
10. Kusababisha kutia mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
11. Kulala nje ya shule bila ruhusa.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruaga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kuwa na simu ya mkononi au kutumia simu ya mkononi bila ya ruhusa ya mwalimu.
15. Kutoingia darasani na kutokufanya kwa makusudi mitihani, majaribio na mazoezi yatolewayo na walimu, Wilaya na Mkoa.
16. Makosa mengine ya utovu wa nidhamu, ukiukaji wa maadili na jinai.

MKUU WA SHULE
SHULE YA UFUNDI B[illegible]
MWANZA

**KIAMBATANISHO NYONGEZA B**

**MEDICAL EXAMINATION FORM DATE ……………………………………**

**NAME OF STUDENT ………………………………….**

**To medical officer I/C of…………………………………… District/Regional/Referal Designated Hospital, P.O.BOX …………………………**

**Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for being able to pursue two year of Secondary school education. The examination should include categories a – p. In case of an acute or defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligble of admission to schools of students with special needs.**

**(a) Eye sight ……………………………………………………………………………..**
**(b) Heart examination……………………………………………………………………**
**(c) Blood pressure……………………………………………………………………….**
**(d) Chest X-Ray …………………………………………………………………………**
**(e) Hearing………………………………………………………………………………**
**(f) Speech……………………………………………………………………………..**
**(g) Venereal Disease …………………………………………………………………….**
**(h) Leprosy ………………………………………………………………………………**
**(i) Eplapay ………………………………………………………………………………**
**(j) Stool routine …………………C/S………………………………………………………**
**(k) Urine routine…………………………C/S……………………………………………**
**(l) Sickle cell test ……………………………………………………………………….**
**(m) WBC total Differential……………………………………………………………..**
**(n) OBP including ESR………………………………………………………………….**
**(o) FOB ………………………………………B/S……………………………………………..**
**(p) Others …………………………………………………………………………**

**NAME…………………………………… SIGNATURE………………………….**
**DESIGNATION…………………………**

**OFFICIAL STAMP………………………………. DATE……………………………**

**Bandika picha moja ya mwanafunzi hapa, Awe na shati jeupe la shule.**

**KIAMBATANISHO NYONGEZA C.**

**HISTORIA NA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

**1.MAELEZO BINAFSI:**

**(a) Jina la mwanafunzi …………………………………………………………..**

**(b) Majina ya wazazi i) Baba ……………………………………………Hai/amefariki**

**ii) Mama ……………………………………...Hai/amefariki**

**(c) Kabila la mwanafunzi ………………………………………………………………**

**(d) Tarehe ya kuzaliwa (mwanafunzi)………………………… mkoa ………………….**

**Wilaya ……………………….. Tarafa ………………………… Kata ………………**

**Kijiji ………………………………… alikozaliwa**

**(e) Ni raia wa ………………………………………….**

**(f) Jina la mlezi ( kama anatunzwa na mlezi) …………………………………………**

**(g) Uhusiano na mlezi ………………………………………………………………**

**kazi ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………….**

**(h) Sehemu/ofisi anayofanyia kazi mzazi/mlezi ………………………………………**

**(i) Matatizo maalumu aliyonayo mwanafunzi ……………………………………….**

**2: SHULE ALIZOSOMA.**

| **Na.** | **SHULE** | **WILAYA/NCHI** | **MADARASA** | **MWAKA WA KUANZA NA KUMALIZA** | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

**3: MAELEZO YA NYONGEZA KAMA YAPO.**

**……………………………………………………………………………………………**

Saini ya Mwanafunzi …………………………………………... Tarehe …………………

4: **KUPOKELEWA SHULENI** ( itajazwa shuleni)

Tarehe aliyopokelewa shuleni……………………………Kidato……………………….

Nambari ya Usajiri ………………………………………

**KIAMBATANISHO NYOGEZA D:**
**NDUGU WATAKAO MTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI:**

Mzazi/Mlezi wa …………………………………… Kidato ………………. 20…………
Utaratibu wa shule unawaruhusu wazazi/walezi na ndugu wasiozidi watatu utakaowachagua wewe mwenyewe kufika shuleni kumjulia hali kijana wako. wageni hawaruhusiwi kufika shuleni miezi ya mei na novemba kwa sababu ya kuwepo mitihani hapa shuleni. Ni vyema wageni wafike saa za masomo kuweza kupata fursa ya kuonana na mwalimu wa darasa la mtoto ili kumjulia maendeleo yake ya kitaaluma.

| TAARIFA | Ndugu wa kwanza | Ndugu wa pili | Ndugu wa tatu |
|---|---|---|---|
| Jina la ndugu | | | |
| Kazi yake | | | |
| Uhusiano naye | | | |
| Anakoishi | | | |
| Anuani yake | | | |
| Simu yake | | | |

Nimeelewa maelezo hayo hapo juu, Nina maoni yafuatayo ( Eleza kama yapo ):-
………………………………………………………………………………………………
Jina la Mzazi/mlezi ………………………………………………………………
Saini ya mzazi/Mlezi ……………………………………… Tarehe
………………………

**KIAMBATANISHO NYOGEZA E:**
**AHADI YA KUTII SHERIA /AMRI NA MAMLAKA YA SHULE:**

1. Mimi Mwanafunzi…………………………………………… Nimesoma kwa makini sheria zote za shule na nyongeza yake. Nimezielewa barabara na ninakubali kwa hiari yangu kuzitii na kuziheshimu. Nitafanya kazi na kusoma kwa bidii ili kujijengea msingi bora wa maisha yangu ya badaae ili kujiletea heshima na sifa yangu binafsi na shule yangu kwa ujumla.
   Ndimi mwanafunzi (Jina)
   …………………………………………………………………………
   Saini …………………………. Tarehe ………………………

2. Mimi …………………………………. Mzazi/Mlezi nimesoma sheria na taratibu za shule, Nimezielewa na mimi nakubali kijana wangu ajiunge na masomo katika shule hii.

Ndimi Mzazi/Mlezi (Jina)
……………………………………………………………….
Anuani ya kudumu:
………………………………………………………………………………………
…
Saini ……………………….simu………………………………
Tarehe……………………

**NAKUTAKIA SAFARI NJEMA NA KARIBU SANA BWIRU WAVULANA**

**SAINI YA MKUU WA SHULE:**

